

MAMBO MUHIMU KUHUSU UKOMA

- Ukoma ni ugonjwa unasababishwa na vimelea aina ya bakteria.
- Ukoma siyo ugonjwa wa kulogwa wala kurithi.
- Ukoma huambukizwa kwa njia ya hewa
- Kwa kawaida ukoma huathiri sehemu za ngozi na mishipa ya fahamu.
- Dalili kuu ni baka au mabaka ambayo hukosa hisia ya joto, mguso au maumivu
- Mgonjwa wa ukoma akiwahi kufika kwenye matibabu atatibiwa na kupona kabisa.
- Ugonjwa huu usipotibiwa mapema hugaribu mishipa ya fahamu na kusababisha ulemavu wa kudumu
- Ukoma unatibiwa kwa mchanganyiko wa dawa maalum za MDT ambazo zinapatikana katika vituo vyote vya tiba vikiwemo vya serikali, mashirika ya dini na baadhi ya Zahanati za watu binafsi.
- Tiba ya ukoma inachukua kati ya miezi sita hadi mwaka mmoja kulingana na ushauri wa Mganga.
- Mgonjwa anashauriwa kunywa dawa alizopewa kila siku bila kukosa ili apone kabisa.
- Mgonjwa ambaye ameanza tiba hawezi kumuambukiza mtu mwingine na hivyo hakuna sababu ya kumtenga.
- Mgonjwa ambaye yuko kwenye tiba ya ukoma anaweza kuendelea na taratibu za kawaida za maisha yake.